



United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

Ujumbe kutoka kwa Bi. Irina Bokova, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kusoma na Kuandika, 8 Septemba 2017

Kusoma na kuandika katika ulimwengu wa Kidijitali.

Teknolojia ya dijitali imepenyeza katika nyanja zote za maisha yetu, kimsingi imebadilisha namna tunavyoishi, kufanya kazi, kujifunza na kushirikiana.

Teknolojia hizi mpya zinafungua fursa mpya za kuboresha maisha yetu na kutuunganisha kiulimwengu - lakini pia zinaweza kuwatenga wale ambao hawana ujuzi muhimu wa kuzitumia, kama vile ujuzi wa kusoma na kuandika unavyowatenga.

Kijadi, kusoma na kuandika imekuwa ikichukuliwa kuwa seti ya ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu ambayo hutumika katika muktadha fulani. Jamii ya kidijitali inabadili maana ya kusoma na kuandika, ikihitaji viwango vya juu zaidi vya ujuzi huu. Wakati huo huo, teknolojia inaweza kutumika ili kuboresha ujuzi wa kusoma na kuandika.

Hili halina budi kueleweka katika muktadha mpana zaidi. Ulimwenguni kote kwa sasa, watu wazima wapatao milioni 750 bado hawana ujuzi wa msingi wa kusoma na kuandika. Watoto na vijana wapatao milioni 264 hawana nafasi ya kufaidika na elimu shuleni. Aidha, utafiti wa kimataifa unaonyesha kwamba sehemu kubwa ya watu wazima na vijana duniani kote, ikiwa ni pamoja na nchi zilizoendelea, hawana ujuzi wa msingi wa dijitali unaohitajika ili kufanya kazi kikamilifu katika jamii za leo na mahali pa kazi. Kupunguza pengo hili la ujuzi ni sharti muhimu la kielimu na kimaendeleo.

Teknolojia ya habari na mawasiliano inatengeneza nafasi ya kukabiliana na changamoto hii. Vifaa vya kidijitali vinaweza kupanua nafasi za kujifunza na kuboresha namna ya kujifunza. Nyezo hizi zinaweza kutumika kuwafikia wale ambao katika hali ya kawaida wasingeliweza kufikiwa, kufuatilia mwenendo wa mafunzo, kuwezesha tathmini ya ujuzi, na kufanya usimamizi na utawala wa mifumo ya utoaji ujuzi kuwa na ufanisi zaidi.

Ili tuweze kujenga na kuchukua fursa mpya za kuendeleza Lengo la Maendeleo Endelevu namba nne juu ya Elimu na kujifunza kwa wote, tunahitaji hatua ya pamoja. Ushirikiano kati ya serikali, mashirika ya kiraia na sekta binafsi ni muhimu katika kukuza kusoma na kujifunza katika ulimwengu wa kidijitali. Ninaona ushirikiano wa kimataifa kwa ajili kueneza ujuzi wa kusoma na kuandika (Global Alliance for Literacy) katika Mfumo wa Mafunzo ya Elimu Endelevu kama mfano wa jitihada za pamoja ambazo tunahitaji ili kuendeleza ajenda ya kimataifa na kusaidia mipango ya kitaifa ya kujifunza kusoma na kuandika.

Siku ya Kimataifa ya Kusoma na Kuandika hutoa muda wa kutafakari maendeleo na kujumuika pamoja ili kukabiliana na changamoto zilizoko mbele yetu. Mwaka huu, maadhimisho haya yamejikita katika kuelewa vizuri aina ya elimu ya kusoma na kuandika inayohitajika katika ulimwengu wa kidijitali ili kujenga jamii shirikishi, zenye usawa na endelevu. Kila mtu anapaswa kufaidika zaidi na kipindi hiki cha kidijitali, ili

kundeza haki za binadamu, majadiliano na kubadilishana mawazo, na kukuza maendeleo endelevu.